JANUARI -DESEMBA 2005

Mtazamo wa UN & ILO; ugumu wa ajira, vigingi maendeleo vilivyokuwa duniani



BUFE

IJUMAA DESEMBA 26, 2025

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




WASAFIRISHAJI NA RABSHA ZA MWANZO, MWISHO MWAKA...

# LATRA yazuru katika mikoa kwa elimu na kurekebisha mapengo




Maofisa wa LATRA makao makuu, Dodoma na mkoani Songwe, pia wadau wengine wa barabarani walipoendesha semina elekezi kwa madereva na wamiliki wa vyombo vya moto mkoani Songwe. Picha nyingine chini ni wanaofuatlia darasa; askari wa usalama barabarani, madereva na wamiliki wa vyombo vya moto. **PICHA ZOTE: IBRAHIM YASSIN.**

**NA IBRAHIM YASSIN, SONGWE**

TANGU kufika tarehe za mwisho wa mwaka kuziona siku kama jana na leo, kuelekea kufungua mwaka, kuna pilika nyingi za kusafiri watu kuelekea makwao, kisha wanatarajiwa kurudi wanakoendesha maisha ya kila siku.


Hiyo hali zaidi iko hasa katika mikoa ya Kaskazini mwa nchi, toleo la jana la gazeti hili likawa na habari namna mjini Moshi mkoani Kilimanajaro kulivyofurika watu waliorejea nyumbani.

Inaelezwa kwamba, kuwapo hali hiyo huendana na vyombo vya usafiri na hasa mabasi, kupandisha nauli, kujaza abiria kupita kiasi katika magari yanayosafiri umbali mrefu, mathalan katik ya mikoa.

Ni mustakabali unaotajwa kuhatarisha usalama wa abiria, hata kufikia ajali za kila mara kwa mara imebainika.

Imekuwa kawaida kwa wanaohudumia vyombo vya moto wengi,siku za sikukuu wanazitumia kama fursa kujipatia kipato kikubwa, wakivunja sheria kwa kupandisha nauli na kujaza abiria kupita kiasi, pasipo kujali upande wa pili wa madhara ya ajali.

Miaka yote inapofika mwisho mwa mwaka katika sikukuu za Krismasi na mwaka mpya, kumeshuhudiwa ajali za kila mara zinazosababishwa na uzembe na tamaa ya madereva na makondakta wao.



Katika maeneo mengi ya stendi za mabasi yaendayo mikoani, zimekuwa zikifanyika baada ya wakatisha tiketi kupandisha nauli, baada ya kuwapo abiria wengi wanaoenda mapumzikoni na hata shule zinapofunga.

Kwa wamiliki wa vyombo vya moto, pia wamekuwa wakilalamikiwa kukosa elimu na matumizi sahihi ya ving'amuzi, wakiwalalamikia madereva wa magari, pindi wanapoona gari linatozwa faini za kila mara.

**LATRA YACHUKUA HATUA**

Kutokana na kuwapo makosa, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kupitia maofisa wake wa kitengo cha sheria makao makuu, sasa wanatoa semina elekezi kwa madereva wa vyombo vya mto na wamiliki, sehemu mbalimbali ili kuondoa changamoto za ajali barabarani.

Walikuwa mkoani Songwe hivi karibuni, wakitokea Rukwa kwa semina elekezi za maofisa usafirishaji, madereva wa vyombo vya moto na wamiliki wake.

Ni mafunzo yaliyofanyika katika ukumbi wa Jeshi la Polisi - Usalama Barabarani, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, maofisa LATRA mikoa na taifa, zikiwalenga maofisa wa LATRA, wamiliki wa vyombo vya motoa mikoa na taifa, hali madereva wa vyombo vyote vya moto, kama; magari, pikipiki na bajaji.

Akifungua kikao, Meneja wa LATRA mkoani Songwe, Joseph Bulongo, anasema dhima ya mafunzo hayo ni kukumbushana na kupeana kanuni kuu sita za uendeshaji vyombo vya moto.

Ofisa Sheria wa LATRA kutoka makao makuu Martha Ngaga, anasema baada ya kuona sheria nyingi zinakiukwa, wameamua kupita kila mkoa nchini kukumbushana na kuelezea kuwapo kanuni sita.

Anasema, kanuni hizo zitajulikana kuwa za uwezeshaji watoa huduma za usafirishaji za mamlaka udhibiti na usafiri ardhini za mwaka 2024.

Ofisa Martha, anaongeza kuwa, kanuni hizo zitatumika pia kwa wawezeshaji huduma za za usafirishaji wa abiria na mizigo kupitia mfumo, usimamizi au kwa namna yeyote ya uwezeshaji.

INAENDELEA UK.12

CamScanner




# LATRA yazuru katika mikoa kwa elimu na kurekebisha mapengo

**INATOKA UK.11**

Kwa mujibu wa Martha, Mamlaka ya Udhibiti usafiri Ardhini iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, maana ni mtu au kampuni inayojitegemea kutoa huduma kwa niaba ya mtoa huduma.

Pia, anawaeleza wajumbe hao kuwa mtu atakayekusudia kutoa huduma ya uwezeshaji, anapaswa kuomba kusajiliwa na LATRA, akijaza fomu iliyoainishwa na mamlaka husika.

Lingine analitaja, ni kwa mtoa huduma atakayesajiliwa katika kanuni wezeshi, ataweza kusaidia ukataji tiketi mtandaoni, ili kusaidia kufanya maombi katika mfumo wa leseni za mamlaka, ufungaji vifaa vya kufuatilia mwendo wa chombo, wakala wa mabasi, kukusanya na usambazaji mizigo.

**WAJUMBE WAHOJI**

Mwenyekiti wa Waendesha Bodaboda mkoani Songwe, Omary Mbuba, akaomba ufafanuzi wa msako unaofanywa na LATRA kusaka uhalali wa leseni zao mitaani.

Mbuba anasema, imekuwa kawaida kwa mbia aliyepewa uwakala kuendesha msako mitaani na kukamata pikipiki au bajaji zisizokuwa na leseni, hali inayozua misuguano kati yao.

Elia Kibona, mmiliki wa magari, licha ya kupongeza uendeshaji mafunzo hayo, akawataka maofisa hao kupunguza gharama za faini, huku akiwataka wamiliki wenzake kuona umuhimu wa kufunga ving'amuzi kwenye magari yao.

Naye dereva Sai Padwi, akahoji vigezo vinavyotumiwa na mamlaka husika, kuwatoza faini kati ya shilingi laki tano na milioni moja, pindi wanapowakuta na makosa barabarani, akisisiyiza kuwa faini hizo ni kubwa kuliko makusanyo wanayoyapata.

Elly Songuo Kaimu Katibu wa wamiliki wa magari aina ya Toyota Coaster (mabasi ya abiria 26), akadai kuwa sheria nyingi zinazotungwa na kuwa chini ya LATRA, kwamba sio shirikishi kwao,a pia mazingira ya barabara nyingi ni mbovu.

Mmiliki wa magari makubwa mkoani Songwe, Thobias Maribwa, anasema magari ya kutoka Tunduma kwenda Mbeya, abiria wake wengi wanapandia njiani, lakini wamekuwa wakitozwa faini kwa madai kuwa hawajakata tiketi. Hapo anaomba ufafanuzi wa jambo hilo.

Akizungumzia suala la faini kwa dereva anayeendesha mwendo mkubwa, Anthony Sabasaba, Mkaguzi wa Usalama Barabarani kutoka Ofisi ya Wilaya ya Mbozi, anasema wamekuwa wakikagua kila mara, baada ya kugundua makosa yanayojirudia.

Akasema kwa dereva atakayeendesha mwendo kuanzia spidi 86 hadi 99, kisheria anatozwa faini zake na atakayeendesha spidi 100 na zaidi,kisheria kuna adhabu yake ya kunyang'anywa leseni.

Kwa mujibu wa Sabasaba, faini hizo zimewekwa ili madereva waongeze umakini wa kazi barabarani.

Meneja wa LATRA mkoani Songwe, Joseph Bulongo, anasema licha ya kuwapo faini kubwa, mamlka husika imekuwa ikitoza faini za chini zinalizlipika katika hatua ya kumrekebisha mhusika, huku mmiliki wa chombo anapatiwa taarifa ya kosa liliobainika.

Rai yake ni kwa mmiliki wa chombo cha miti kujifungia aliko king'amuzi, ili kutambua nyendo za lake, hata dereva anapotozwa faini, mmiliki atatambua kosa lililotokea akiwa nyumbani.

Anaongeza kuwa, kwa mmiliki anayetaka kufunga king'amuzi na kupewa leseni, anatakiwa kufika katika ofisi za LATRA, ili apewe utaratibu stahiki, ikianza na kujaza fomu na kuelezwa namna ya kulifuatilia gari lake liliko.

Irene Sawe, Ofisa Sheria wa LATRA Mkoa Songwe, anasisitiza umuhimu wa madereva na makondakta kufuata sheria na kanuni zilizowekwa, ili kuepuka kutozwa faini kila wakati.

Kumrejea, Martha Ngaga, Ofisa Sheria LATRA anayetoka makoa makuu, Dodoma anasema: "Ni kosa kwa mtu au kikundi kilichopewa uwakala wa kukatisha leseni za vyombo vya moto, kufanya msako wa kukamata chombo chochote."

Anasema, wakala anayepewa kazi ya kukudanya mapato, anatakiwa kukaa ofisini kwake kukatisha leseni na si kuzunguka mitaani kukamata pikipiki au bajaji.

Hapo anasisitiza kuwa, suala la kuwapo na wanaova sare na kutoza au nembo za LTRA nikosa, akihimiza ni kosa kisheria.

Katika hilo, Martha anawataka madereva kuwa makini na kwa kutowapatia waendesha magari vishoka wasio kuwa na leseni siku za Jumamosi na Jumapili, inasababisha ajali na uvunjifu wa kanuni zilizowekwa kisheria.

> **Pia, anawaeleza wajumbe hao kuwa mtu atakayekusudia kutoa huduma ya uwezeshaji, anapaswa kuomba kusajiliwa na LATRA, akijaza fomu iliyoainishwa na mamlaka husika.**